JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI

# MWONGOZO WA UKUSANYAJI NA ULIPAJI WA ADA YA HUDUMA ZA UMWAGILIAJI NA TOZO YA UREJESHAJI WA GHARAMA ZA UWEKEZAJI KATIKA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI





**JUNI 2020**

## YALIYOMO


YALIYOMO ..... i

DIBAJI ..... ii

FASILI ..... ii

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 VIWANGO VYA ADA, UKADIRIAJI NA IDADI YA WAMWAGILIAJI ..... 2

2.1 Viwango vya ada ..... 2

2.2 Ukadiriaji viwango vya ada ..... 2

2.3 Takwimu za idadi ya wakulima wamwagiliaji ..... 3

3.0 UKUSANYAJI, USIMAMIZI, UIDHINISHAJI NA MATUMIZI YA FEDHA ZA ADA ..... 5

3.1 Ukusanyaji wa ada ..... 5

3.2 Akaunti maalumu ya ada ..... 5

3.3 Uidhinishaji wa matumizi ya fedha ..... 5

3.4 Matumizi ya fedha za ada ..... 6

4.0 WAJIBU WA KULIPA, ULIPAJI ADA KWENYE MFUKO WA MAENDELEO YA UMWAGILIAJI, MGAWANYO WA ADA, SKIMU KUSHINDWA KULIPA NA ADHABU ..... 6

4.1 Nani anawajibika kulipa ada ..... 6

4.2 Ulipaji wa ada kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji ..... 7

4.3 Mgawanyo wa fedha ..... 7

4.4 Skimu kushindwa kukusanya ada kwa kutokuwa na takwimu sahihi za uzalishaji . 7

4.5 Adhabu kwa kuchelewesha malipo ya ada ..... 8

5.0 UKAGUZI WA HESABU ZA FEDHA ..... 8

5.1 Wakaguzi wa hesabu za fedha ..... 9

6.0 MAREKEBISHO YA MWONGOZO ..... 9

## DIBAJI

Mwongozo wa ukusanyaji na ulipaji wa ada ya Huduma za Umwagiliaji, unaweka utaratibu wa namna ambavyo ada itatozwa na vyama vya wamwagiliaji kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji za mwaka 2015 iliyochapishwa katika Gazeti la serikali GN Na. 402 la tarehe 11/9/2015. Mwongozo huu umeainisha Ada ya asilimia tano (5%) kama Ada ya Huduma za Umwagiliaji ya wastani wa uzalishaji kwa ekari kwa kila msimu. Asilimia sabini na tano (75%) ya Ada hii itakuwa kwa ajili ya huduma ya Uendeshaji na Matunzo ya skimu na asilimia ishirini na tano (25%) itaingizwa kwenye Mfuko wa Maendeleo wa Umwagiliaji "*Irrigation Development Fund" (IDF).*

Vilevile, Mwongozo huu unaweka utaratibu wa namna ambavyo Tozo ya urejeshaji wa kiasi cha gharama za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji iliyogharamiwa na Serikali itakavyotozwa (kifungu 52(2) (b) cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013).

Aidha, Mwongozo huu utatumika kwa skimu zote za umwagiliaji zilizoboreshwa na kuendelezwa.

## FASILI

Katika Mwongozo huu, fasili ya maneno yaliyotumika ni kama ifuatavyo:-

| Maneno | Fasili |
|---|---|
| ***Ada ya Huduma za Umwagiliaji ni:*** | Ada inayolipwa au kukusanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 39 cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013 kwa lengo la kukidhi gharama za uendelezaji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji. |
| ***Huduma za Umwagiliaji ni:*** | Shughuli au kazi zote zinazolenga kuboresha uendelevu wa skimu za umwagiliaji zikijumuisha upembuzi yakinifu, utafiti, usanifu, ujenzi, uendeshaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji na kujenga uwezo wa wamwagiliaji |
| ***Skimu ya umwagiliaji ni:*** | Eneo ambalo linastawisha mazao kwa aina yeyote ya umwagiliaji, uwe wa matone au kunyunyizia au wa wazi ikiwa ni pamoja na mifumo |

| | |
|---|---|
| | inayotumia maji yanayotiririka kwa nguvu ya mvutano wa ardhi au kusukumwa kwa pampu kuingia kwenye mifereji au mabomba kutoka kwenye chanzo wazi au chini ya ardhi, au maji ya mvua yaliyovunwa |
| ***Skimu ya umwagiliaji iliyoboreshwa ni:*** | Skimu ya umwagiliaji ambayo imejengwa au kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji kitaalamu |
| ***Vyama vya wamwagiliaji ni:*** | Muungano wa wakulima wenye nia moja ya kuendeleza au kuendesha kilimo cha umwagiliaji katika skimu kwa lengo la uendelezaji na usimamizi madhubuti wa skimu za umwagiliaji. |
| ***Tozo ya kurejesha gharama za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ni:*** | Tozo inayolipwa au kukusanywa kwa mujibu wa kifungu 31(e) cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 ya Mwaka 2013 kwa lengo la kurejesha kiasi cha gharama za ujenzi wa miundombinu ya miradi ya umwagiliaji ambayo Serikali imewekeza. |

## 1.0 UTANGULIZI

Kilimo cha umwagiliaji hapa nchini kwa muda mrefu kimekuwa kikikabiliwa na changamoto mbalimbali. changamoto hizo ni pamoja na hali duni ya uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji ambapo wakulima wanashindwa kutambua na kutekeleza wajibu wao kikamilifu katika kuchangia ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ambayo imejengwa na serikali au wadau wa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji kwa fedha nyingi, hali hii imesababisha miundombinu ya umwagiliaji kukosa uendelevu.

Serikali vilevile inawajibika kuendelea kupanua eneo la umwagiliaji katika maeneo mengine ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji hivyo wakulima wamwagiliaji wanawajibika kurejesha gharama za uwekezaji ili serikali iendelee kuwekeza katika maeneo engine ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji nchini.

Aidha, vyama vingi vya wamwagiliaji havina mifumo madhubuti ya ukusanyaji na ulipaji wa ada ya Huduma za Umwagiliaji. Hata vyama ambavyo vina mifumo ya ukusanyaji na ulipaji wa ada bado havina usimamizi thabiti. Ukosefu wa usimamizi madhubuti wa fedha kwenye vyama vya wamwagiliaji husababisha migogoro ya mara kwa mara miongoni mwa wamwagiliaji. Hitaji la Mwongozo huu limetokana na kuwepo kwa hali duni ya uendeshaji, utunzaji wa miundombinu na ukosefu wa usimamizi madhubuti wa fedha zinazokusanywa.

Hivyo, ili wamwagiliaji waweze kutumia, kusimamia na kuendesha miundombinu ya umwagiliaji kikamilifu wanahitaji kuiendesha na kuitunza kwa mujibu wa mwongozo huu. Mwongozo umeainisha viwango vya ada na tozo, ukadiriaji wa wastani wa uzalishaji, ukusanyaji wa ada na tozo, sharti la kufungua akaunti maalumu, matumizi ya ada na tozo, sehemu ya ada itakayowekwa kwenye mfuko wa maendeleo ya umwagiliaji, ukaguzi wa hesabu za fedha, ulipaji wa ada na tozo kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji na adhabu kwa ada iliyocheleweshwa kulipwa.

Mwongozo huu umeandaliwa mahsusi kwa ajili ya wamwagiliaji, viongozi wa vyama vya wamwagiliaji, wataalamu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, wawezeshaji wa vyama vya wamwagiliaji, wataalamu pamoja na wadau katika sekta ya umwagiliaji.

Matokeo yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa Mwongozo huu ni kuwa na:

i. Miundombinu ya umwagiliaji inayotumika kutunzwa vizuri kwa uendelevu;

ii. Kuweka/kuimarisha mfumo madhubuti wa ukusanyaji na ulipaji wa ada;

iii. Mfumo wa wazi katika usimamizi mzuri wa fedha na

iv. Uwekezaji wenye tija katika sekta ya umwagiliaji.

# 2.0 VIWANGO VYA ADA NA TOZO, UKADIRIAJI NA IDADI YA WAMWAGILIAJI

## *2.1 Viwango vya ada*

Katika kila skimu ya umwagiliaji kila mkulima wa umwagiliaji anawajibika kutoa ada ya huduma za umwagiliaji ambayo ni asilimia tano (5%) ya wastani wa uzalishaji kwa ekari kwa kila msimu na ya asilimia kumi (10%) ya wastani wa uzalishaji kwa ekari kwa kila msimu ikiwa ni Tozo ya kurejesha kiasi cha gharama za ujenzi wa miundombinu ya miradi ya umwagiliaji ambayo Serikali imewekeza.

## *2.2 Ukadiriaji viwango vya ada na tozo*

Baada ya mavuno kamati au Bodi za usimamizi za vyama vya wamwagiliaji kwa kusaidiana na wataalamu wa kilimo, watakokotoa wastani wa uzalishaji uliofikiwa kwa ekari kwa kila zao linalolimwa katika skimu na kupata kiwango cha ada na tozo. Kiwango cha uzalishaji kilichopendekezwa na kamati ya usimamizi kitawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa chama cha wamwagiliaji. Kiwango cha ada kilichokokotolewa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa chama cha wamwagiliaji ndicho kitalipwa katika msimu husika.

### *2.3 Takwimu za idadi ya wakulima wamwagiliaji*

Kamati za usimamizi za vyama vya wamwagiliaji zitaandaa orodha ya idadi ya wakulima ambao wamelima katika msimu huo pamoja na eneo lililolimwa. Aidha, kamati za usimamizi za vyama zitatakiwa kuwa na orodha ya umiliki wa mashamba ambayo itaonesha kila mkulima na ukubwa wa maeneo anayomiliki. Kupitia takwimu hizi itawezesha makusanyo stahiki kufanyika. Takwimu hizo zitajazwa katika Fomu Na. 1 kama inavyoonekana hapa chini.

*Fomu Na. 1*:

**Jina la Skimu..........................................................................................................................................**

**Wilaya......................................................Mkoa…………….............................................................................**

**Msimu na mwaka……………………………………………………………………………………..**

| **Na.** | **Jina la Mkulima** | **Jinsi** | **Umri** | **Kitongoji** | **Mfereji/ Kitalu** | **Mazao yaliyolimwa ( Ekari)** | | | **Jumla ya eneo lililolimwa** | **Jumla ya eneo linalomilikiwa** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Mpunga | Vitunguu | Mazao mengine | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |

**Fomu Na. 1.** Itakapokamilika itatunzwa kwenye ofisi ya chama cha wamwagiliaji na nakala zitawasilishwa kwenye Ofisi ya Mkoa na Ofisi za Mamlaka za Serikali za mitaa.

## 3.0 UKUSANYAJI, USIMAMIZI, UIDHINISHAJI NA MATUMIZI YA FEDHA ZA ADA NA TOZO

### *3.1 Ukusanyaji wa ada na tozo*

Ada ya Huduma za Umwagiliaji na Tozo ya Urejeshaji wa Gharama za Ujenzi wa Miundombinu itakusanywa na chama cha wamwagiliaji katika skimu husika. Kila chama kitakuwa na vitabu maalumu ili kuwezesha utunzaji mzuri wa kumbukumbu za fedha.

Ada na tozo zitalipwa wakati wa mavuno kulingana na makubaliano yatakayofanywa katika vikao vyao halali, kama wataamua kulipa baada ya msimu ulipaji wa ada na tozo ufanyike ndani ya miezi miwili baada ya mavuno. Mkulima aliyelipa ada na tozo ikiwa ni mazao au fedha atapewa stakabadhi ili kuthibitisha malipo yaliyofanyika.

### *3.2 Akaunti maalumu ya ada*

Kwa mujibu wa aya ya 84 (3) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), fedha za ada ya Huduma za Umwagiliaji zitatunzwa katika akaunti maalumu ambayo itakuwa ni ada hiyo tu. Akaunti hiyo ndiyo itakayokuwa inasimamia mfuko wa uendeshaji na utunzaji wa skimu kwa ujumla.

Tozo ya Urejeshaji wa Gharama za Ujenzi wa Miundombinu italipwa kwenye akaunti ya Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji.

### *3.3 Uidhinishaji wa matumizi ya fedha*

Ili kuwa na uwazi na kuimarisha uthibiti wa matumizi sahihi ya fedha ya ada ya umwagiliaji, kutakuwa na makundi mawili ya watia saini, Kundi la kwanza ni (i) Mhandisi wa Umwagiliaji wa Wilaya (DIE) na Afisa Kilimo Umwagiliaji na Ushirika (DAICO) wa Halmashauri husika na Kundi la pili ni (ii) Mwenyekiti na Mtunza Fedha wa chama cha wamwagiliaji. Utaratibu huu utawezesha kuwa na uwazi utakaopelekea kuwa na matumizi mazuri ya fedha kulingana na makusudio ya huduma ya Uendeshaji na Matunzo ya Skimu.

### *3.4 Matumizi ya fedha za ada*

Ada ya huduma za umwagiliaji katika skimu za umwagiliaji zinaweza kutumika kugharamia masuala yafuatayo: -

i. Kulipa Ada ya matumizi ya maji kwenye ofisi ya bonde la maji husika;
ii. Uendeshaji na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji;
iii. Ukarabati wa miundombinu iliyochakaa;
iv. Uendeshaji wa magari na mitambo ya chama cha wamwagiliaji;
v. Ununuzi wa zana na vifaa vya kufanya usafi (mf. mashine za kukata nyasi yaani mowers n.k.) na matengenezo ya miundombinu na
vi. Shughuli mbalimbali za utawala pamoja na matumizi mengineyo kadri yatakavyoidhinishwa na mkutano mkuu wa chama cha wamwagiliaji.

## 4.0 WAJIBU WA ULIPAJI ADA KWENYE MFUKO WA MAENDELEO YA UMWAGILIAJI, MGAWANYO NA ADHABU KWA VYAMA VITAKAVYOSHINDWA KULIPA

### *4.1 Nani anawajibika kulipa ada*

Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji (2013), kifungu cha 28 (2) (b) na 29 (2) zinaeleza kuwa itakuwa ni wajibu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Serikali za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na vyama vya wamwagiliaji kuhakikisha kuwa wakulima wote wanao miliki ardhi ndani ya skimu ya umwagiliaji wanakuwa wanachama wa chama cha umwagiliaji na watawajibika kutekeleza sheria ndogo za vyama.

Kwa mujibu wa aya ya 84 (1) (2) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), inaeleza kuwa kila mkulima anayenufaika na Huduma za Umwagiliaji anatakiwa kulipia ada ya huduma kwa chama cha wamwagiliaji. Kwa kuzingatia vifungu hivi viwili na kanuni hiyo, wakulima wote wenye kumiliki maeneo katika skimu za umwagiliaji wanawajibika kulipa ada ya Huduma za Umwagiliaji kwa mujibu wa sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015.

### *4.2 Ulipaji wa ada kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji*

Katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kufanyika ukaguzi wa hesabu za fedha, chama kitawasilisha asilimia ishirini na tano (25%) ya fedha za ada ya Huduma za Umwagiliaji zilizokusanywa na zitawekwa kwenye akaunti ya Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Umwagiliaji. Kila mwisho wa mwaka chama kitawasilisha taarifa ya ukaguzi, kwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

### *4.3 Mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji na huduma ya Uendeshaji na Matunzo*

Kifungu cha 52 cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, 2013 kinaanzisha mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji ambapo fedha zake zitapatikana kutokana na vyanzo mabalimbali ikiwa ni pamoja na ada na tozo mbalimbali. Kwa mujibu wa Kifungu cha 52 (2)(b) kinaeleza kuhusu urejeshaji wa gharama za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; na vilevile kifungu cha 52(2)(e) kinaelezea kuhusu ada ya Huduma za Umwagiliaji.

Aidha, kwa mujibu wa aya ya 84 (2) ya Kanuni za Umwagiliaji, 2015 inaelekeza kwamba fedha za Ada ya Huduma za Umwagiliaji zitagawanywa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** Mgawanyo wa fedha za ada ya Huduma za Umwagiliaji

| **Na** | **Mgawanyo wa fedha za Ada ya Huduma za Umwagiliaji** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| **1** | Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji | 25 |
| **2** | Huduma ya matunzo na Matengenezo ya skimu | 75 |

Baada ya kufunga hesabu zake za msimu husika, kila chama cha wamwagiliaji kitalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya fedha hizo katika Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji.

### *4.4 Skimu kushindwa kukusanya ada na tozo kwa kutokuwa na takwimu sahihi za uzalishaji*

Mazingira kama haya iwapo yatajitokeza katika skimu mojawapo, wataalamu wa kilimo wakutane na wakulima kukubaliana wastani wa mavuno katika skimu husika kabla ya kuanza kwa utaratibu wa ada na tozo hizi ili kupanga kiasi kitakachotumika

kwa eneo linalomilikiwa na skimu. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaweza kuweka wakala wa kukusanya ada na tozo husika kwa makubaliano maalumu kutoka katika skimu ambayo itashindwa kufanya hivyo.

*4.5 Adhabu kwa kuchelewesha malipo ya ada* Kwa mujibu wa aya ya 85 (1) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), inaeleza kuwa, Waziri anaweza kutoa adhabu kwa **kila mkulima wa umwagiliaji aliyechelewa** kulipa ada kamili ya Huduma za Umwagiliaji kwa wakati. Adhabu ya ucheleweshwaji wa mawasilisho ya malipo ya ada itakuwa kama ifuatavyo: -

i. Mwezi 1 - 3, asilimia mbili (2%) ya kiasi cha ada husika

ii. Miezi 4 - 6, asilimia tano (5%) ya kiasi cha ada husika; na

iii. Miezi 7 -12 asilimia kumi (10%) ya kiasi cha ada husika.

Kwa mwanachama ambaye atakuwa halipi ada atafungiwa huduma na uongozi wa chama husika; au anyang'anywe shamba likodishwe kwa mwingine hadi atakapolipa deni lake, mwanachama atarejeshewa huduma iwapo atalipa deni analodaiwa.

## 5.0 UKAGUZI WA HESABU ZA FEDHA

Katika kuhakikisha kwamba fedha zinazokusanywa kwenye vyama vya wamwagiliaji zinatumika ipasavyo; Kwa mujibu wa aya ya 21 (3) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), inaeleza kuwa hesabu za vyama vya wamwagiliaji zitakaguliwa kila mwisho wa mwaka wa fedha. Kazi hiyo itafanywa na wakaguzi walio sajiliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) na kupitishwa na Mkutano Mkuu na kuridhiwa na Mkurugenzi Mkuu.

Aidha, kwa mujibu wa aya ya 21 (4) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), inaelekeza kwamba kila chama cha wamwagiliaji kitatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa kila mwisho wa mwaka wa fedha. Ukaguzi wa hesabu za fedha utawezesha vyama vya wamwagiliaji kuchunguza mwenendo mzima wa vitabu vya hesabu pamoja na kumbukumbu zote ili kuona kama fedha zimetumika kama iliyokusudiwa. Ukaguzi utawezesha: -

i. Kufanya ufuatiliaji wa shughuli ambazo zinafanywa na chama cha wamwagiliaji ili kuthibitisha hali ya fedha katika chama;
ii. Kuweka uwazi katika mapato na matumizi ya fedha na kuhakikisha kuwa zimetumika ipasavyo;
iii. Kudhibiti mianya ya wizi au udanganyifu katika masuala ya fedha isitokee au kama imetokea, basi isaidie kurekebisha makosa yasijirudie tena; na
iv. Kuwezesha chama cha wamwagiliaji kujifunza kutokana na mapendekezo na ushauri wa Wakaguzi juu ya usimamizi mzuri wa fedha.

### *5.1 Wakaguzi wa hesabu za fedha*

Kwa mujibu wa aya 21(2) ya Kanuni za Umwagiliaji (2015), inaelekeza kila chama cha wamwagiliaji kinaweza kuajiri/ kukodisha huduma ya kufanya ukaguzi wa hesabu kila mwaka. Kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (*The Accoutants and Auditors Registration* Act) [CAP *286 R.E. 2002*], Wakaguzi watakaoruhusiwa ni wale ambao wameidhinishwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (*NBAA*). Kila mwaka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itasambaza orodha ya Asasi ambazo zimeidhinishwa na NBAA ili kila chama kiwe kinafanya makubaliano na Asasi hizo na kuwezesha kufanyika kwa ukaguzi.

## 6.0 MAREKEBISHO YA MWONGOZO

Mwongozo huu unaweza kufanyiwa marekebisho wakati wowote na katika kipengele chochote inapotokea ulazima wa kufanya hivyo.

................................